# UMOJA WA AFRIKA




*Mwalimu Julius K. Nyerere akipeana mkono na Rais Felix Houphouet-Boigny mjini Abidjan*

# ZIARA YA RAIS HUKO IVORY COAST

Mwalimu Julius K. Nyerere, tarehe 21 Februari, 1968, alianza safari yake ndefu ya kuzitembelea Nchi nne za Afrika Magharibi na Jamhuri ya Muungano wa Nchi za Kiarabu, akifuatana na Mawaziri wawili wa Serikali: Bwana I. M. Bhoke Munanka na Bwana C. Y. Mgonja, pamoja na maafisa wengine wa Serikali, TANU na Afro-Shirazi.

Nchi ya Ivory Coast ni mojawapo ya nchi za Afrika Magharibi alizotembelea Mwalimu. Inalo eneo la maili za mraba 127,500 na kukaliwa na watu 3,700,000. Mji wake mkuu ni Abidjan. Ilipata Uhuru wake mnamo tarehe 7.8.60. Rais wa nchi hiyo ni Bwana Houphouet-Boigny ambaye pamoja na watu wake alimkaribisha Rais wetu kwa shangwe kubwa.



*Maandamano ya magari kutoka kiwanja cha ndege cha Abidjan kuelekea mijini baada ya Mwalimu kuwasili Ivory Coast kwa ziara rasmi ya kiserikali.*



## HOTUBA YA RAIS NYERERE WAKATI WA KARAMU RASMI ABIDJAN, IVORY COAST, FEBRUARI 26, 1968

**Bwana Rais, Wageni Waheshimiwa,**
**Mabwana na Mabibi,**

Mimi na wenzangu tumefurahi sana tangu tumefika Ivory Coast siku tatu zilizopita. Makaribisho ya Serikali yako na ya wananchi wa Ivory Coast yametufanya tujione kama tuko nyumbani. Mmetutunza vizuri sana, na kwa muda mfupi tuliokuwa nanyi mmejitahidi kutuonyesha yale mliyoweza. Kwa hiyo ningependa kuanza hotuba yangu jioni ya leo kwa kutoa shukrani zetu nyingi kwa mapokezi yenu, na kwa mipango mbali mbali mliyotufanyia ya kutufurahisha. Bwana Rais, kwa kweli umetusaidia sana katika kutimiza shabaha yetu ya kuelewa zaidi maendeleo ya nchi hii, nasi tunawashukuru sana kwa jambo hilo.

Makaribisho ambayo sisi Watanzania tumepokelewa nayo katika Ivory Coast yanathibitisha mawazo yetu kwamba, ingawa kuna mataifa mengi katika Afrika, lakini **Afrika ni moja.** Tofauti zilizoko za njia tunazotumia kutafuta maendeleo haziwezi kuubadili umoja wetu, wala hazizuii mataifa yetu mbali mbali kufanya kazi kwa umoja kwa faida yetu wote.

### Lazima tufanye kazi pamoja

Sisi sote tu mataifa mbali mbali yanayojitawala. Hakuna taifa lo lote la Kiafrika lenye haki ya kuingilia mambo ya ndani ya mataifa mengine ya Kiafrika. Na kila taifa lina mamlaka, na wajibu wa kuamua njia gani ya kufuata. Lakini hata hivyo tunaweza kufanya kazi pamoja; na lazima tufanye kazi pamoja.



*Rais Houphouet-Boigny wa Ivory Coast asoma hotuba ya kumkaribisha Rais J. K. Nyerere (wa pili kushoto) kwenye karamu rasmi iliyoandaliwa kwa ajili ya ugeni wa Mwalimu mjini Abidjan.*



## Tofauti zisifanye nchi zetu zichukiane

Kwa mfano, sisi katika Tanzania tumeamua kufuata siasa ya Ujamaa kama Imani yetu; tunajaribu makusudi kujenga taifa la Ujamaa kwa kufuata asili yetu ya Ujamaa vijijini. Tunatambua kwamba kazi tuliyoamua kuifanya ndio kwanza tunaianza, lakini maendeleo tuliyopata mpaka sasa ni ya kujivunia. Kwa upande mwingine wewe, Bwana Rais, umeieleza siasa ya Ivory Coast kuwa "mageuzo ya maisha kwa hiari". Tofauti hizi hazina maana kwamba nchi zetu zichukiane, au hata kuoneana mashaka. Uamuzi huo, ulio tofauti, hautukatazi kushirikiana, kwa kadiri mipaka yetu itakavyoturuhusu. Inawezekana, kwa sababu ya tofauti ya mawazo yetu, ikawako mipango tofauti ya ushirikiano, inayotufaidia sisi sote. Lakini tofauti hizo haziwezi kuudhuru udugu wa Kiafrika, wala kutupa sisi visingizio vya kukwepa haja ya Afrika katika kuutafuta umoja huo. Na kama hivyo ndivyo baina ya Tanzania na Ivory Coast, basi ni kweli vile vile baina ya nchi zingine za Afrika zilizo jirani zaidi.

## Tukitaka kuendelea, tuzikubali tofauti hizo

Tunafahamu kwamba Afrika huru ina nchi zinazojitawala 38; na kila moja katika hizo ni tofauti na nyingine zote. Zile nchi zinazopendelea siasa ya Ujamaa zenyewe zina tofauti katika mipango yao ya siasa na uchumi. Na zile zinazopendelea siasa ya Kibepari, au hata zile zinazosema hazitaki Ujamaa wala Ubepari, pia nazo kila moja ni tofauti na mwenzake. Na wote, jinsi tunavyoendelea kutoka katika hali ya sasa, tutazidi kutofautiana. Tofauti zipo. Tukitaka kuendelea jambo la kufanya ni kuzikubali tofauti hizo.



*Viongozi wawili, Rais Boigny wa Ivory Coast na Mwalimu Julius K. Nyerere watakiana heri katika karamu iliyoandaliwa na Mwalimu Julius K. Nyerere kwa heshima ya mwenyeji wake mjini Abidjan.*




Mambo haya muhimu yanayotakiwa katika kuukuza umoja wetu ni rahisi kuyatamka; lakini kuyatimiza kutaleta mabishano na shida nyingi. Lakini tukiishikilia misingi hiyo tutapiga hatua katika Afrika, hatua itakayotufaidia kila mmoja wetu.

## Tusiwe na uhasama na watu wengine

Kuna jambo jingine moja tu ninalotaka kutilia mkazo kuhusu mwendo wetu wa kuelekea **Umoja wa Afrika,** nalo ni hili. Umoja wetu hauna maana kwamba tuwe na uhasama na watu wengine wa ulimwengu. Mtu kulipenda sana kabila lake au ukoo wake si lazima alichukie taifa lako; wala mtu kuwa raia wa taifa huru la Kiafrika hakumfanyi avunje uaminifu wake kwa Afrika na umoja wake. Vivyo hivyo hatua ya kuelekea umoja katika Afrika si lazima ianzishe uhasama na Ulaya, au Asia, au Amerika. Maana kila mtu anao uhusiano na makundi mengi. Wakati mwingine ana ukoo, na vile vile kabila lake; pia ni rais wa taifa lake, na anaungana na mataifa mengine ya Afrika kupitia Umoja wa Nchi za Kiafrika; na vile vile ni raia wa ulimwengu. Tutake au tusitake, sisi tunahusika na jumuiya zote hizo. Vikundi vyote hivyo vinaendelea vikihusika, na matokeo ya mmoja yanamhusu mwenzake.

## Lakini ndugu huwa upande mmoja

Kwa hiyo hatuwezi kusema kuwa kuipenda zaidi Afrika kuliko nchi zingine zisizo za Afrika lazima kuleta uhasama na nchi zingine, kama vile vile ambavyo mtu kumpenda sana ndugu yake si lazima awachukie jamaa wengine wote wa kijiji chao. Ndugu hutegemeana, hufanya kazi pamoja kwa faida yao wote; na wakipata nafasi ya kuchagua watapendelea kufanya kazi pamoja kuliko kufanya kazi na mtu mwingine. Unapotokea



*Mayor wa Abidjan, Ivory Coast (amevalia ukanda mweupe) ana-ongozana na Mwalimu Nyerere kwenye ukumbi wa mji wa Abidjan.*



ugomvi na watu wengine, ndugu huwa upande mmoja. Wenyewe wanapogombana hupenda kuyamaliza ma-gomvi yao wenyewe; hawataki kabisa kuingiliwa na watu wengine. Yafaa sisi tulio mataifa ya Kiafrika tujiweke katika umoja kama watu wa ukoo mmoja, na kwa kweli ndivyo tulivyo; na halafu tutakapokuwa kundi moja, tutaweza kwa urahisi kufanya kazi na mataifa mengine ya ulimwengu, tukiwa watu sawa.

### Afrika sasa imejifunza

Tumekwisha ianza kazi hii. Nchi zote huru za Kiafrika ni wanachama wa Umoja wa Nchi za Kiafrika, na juu ya shida zilizopatikana katika kuuanzisha umoja huo, naamini kwamba Umoja wetu utatufaa sote katika siku za mbele. Ni kweli kwamba wakati tulipouanzisha umoja wa Nchi za Kiafrika tulijaribu kwenda mbio mno, tukaupa kazi nyingi kuliko kiasi chake, maana tulikuwa bado hatuaminiani sisi kwa sisi. Lakini naamini kwamba Afrika sasa imejifunza kutokana na makosa hayo. Tumejifunza kwamba Umoja wa Nchi za Kiafrika ni ubao wa kwanza tu wa daraja la kuunganisha mataifa yetu. Hatuna budi kuulinda ubao, lakini hatuna budi vile vile kuongeza mbao zingine ili daraja letu liwe imara zaidi kabla ya kupitisha mizigo mizito zaidi juu yake. Tunaweza kuliimarisha daraja hilo kwa mipango mbali mbali ya ushirikiano wa nchi zilizo jirani, na ushirikiano wa kifundi. Lakini kamwe tusisahau shabaha yetu, na wala tusiache mipango yetu ya nchi za jirani ikaharibu au kuondoa mafanikio yetu ya hatima ya umoja katika bara zima.

Bwana Rais, pengine nimetamka maneno mazito mno jioni ya leo. Lakini mimi nadhani kwamba jambo hili la Umoja wa Afrika lina umuhimu ulio sawa kwetu sisi sote; umuhimu wenyewe unazidi tofauti zetu za malezi na ujuzi, maana umoja huo unatuhusu sisi sote.



*Rais Mwalimu Julius K. Nyerere atia sahihi katika kitabu cha wageni cha Abidjan City Council. Mayor wa mji yuko kulia mwa picha akiangalia.*



**Pongezi kwa mafanikio**

Kabla sijakaa kitako kuna jambo moja maalum ninalotaka kusema. Ninapenda kueleza, Bwana Rais, jinsi mimi na wenzangu tulivyofurahi sana katika muda mfupi tuliokaa Ivory Coast. Tumejifunza mambo mengi sana, na tumeshangazwa na maendeleo mlioyafanya. Ni wazi kwamba isingewezekana kwa muda wa siku tatu (na muda mwingine katika huo tumeutumia kwa mazungumzo ya maana) kuona mambo yote ambayo mngeweza kutuonyesha. Lakini tuliyoyaona yanatosha kuelewa maendeleo makubwa ambayo Serikali na watu wa nchi hii wameyafanya. Kwa hiyo kwa niaba ya Tanzania napenda kuwapa pongezi kwa mafanikio yenu.

Bwana Rais, napenda kwa moyo huo kukuomba wewe na wageni waliohudhuria hapa tusimame na kuomba dua la afya: "Kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Ivory Coast, na kwa maendeleo ya Umoja wa Afrika."



*Mayor wa mji wa Abidjan amkabidhi Mwalimu Julius K. Nyerere ufunguo wa mji wa Abidjan na kumpa Mwalimu heshima ya kuwa raia huru wa mji huo.*





*Katika kiwanja cha ndege cha Abidjan Rais Mwalimu Julius K. Nyerere asindikizwa na mwenyeji wake Rais Houphouet-Boigny wakati Mwalimu alipomaliza ziara yake.*

Kimetolewa na Idara ya Habari,
Sanduku la Barua 9142, Dar es Salaam,
na kupigwa chapa na
National Printing Co. Ltd., Dar es Salaam.